IJUE SHERIA YA USHAHIDI NAMBA 9 YA 2016 ZANZIBAR

Sheria ya ushahidi ya Zanzibar ilianza lini kufanya kazi?

Sheria ya Ushahidi namba 9 ya 2016 ya Zanzibar (Sheria ya Ushahidi) ilianza kufanya kazi rasmi mnamo tarehe 18 Januari 2017.

Sheria ya ushahidi ina kazi gani?

Sheria ya Ushahidi ni sheria inayoelekeza utaratibu wa kutolewa na kupokelewa ushahidi mahakamani ili kuthibitisha jambo linalobishaniwa.

Ushahidi unatolewa wapi?

Ushahidi hutolewa katika shauri au kesi yoyote ya madai au ya jinai iliyopo mahakamani kwa nia ya kuthibitisha kuwepo au kutokuwepo kwa tukio linalosemwa kwamba limetokea.

Nani anaweza kutoa ushahidi mahakamani?

Kila mtu anao uwezo wa kutoa ushahidi mahakamani.

Wakati gani mtu huwa hawezi kutoa ushahidi mahakamani?

Ingawa kila mtu anao uwezo wa kutoa ushahidi mahakamani, wakati mwngine mtu anaweza kuzuiwa kutoa ushahidi pale ambapo mahakama inaona kwamba mtu huyo anashindwa kuelewa au kuyafahamu maswali anayoulizwa, au anashindwa kutoa majibu ya msingi kwa maswali anayoulizwa kutokana na mtu huyo kuwa na umri mdogo, au ni mzee sana, au anasumbuliwa na maradhi ya kimwili au kiakili.

Ni yupi shahidi mtoto?

Shahidi mtoto ni yule shahidi ambaye yupo chini ya umri wa miaka 18. Hata hivyo mtoto aliye chini ya umri wa miaka 14 kabla ya kutoa ushahidi wake hutakiwa kupimwa na mahakama kama anatambua umuhimu wa kusema ukweli na kufahamu maana ya kiapo pamoja na athari yake.

Je ushahidi wa mtoto ni lazima uungwe mkono na ushahidi mwengine katika kesi za jinai?

Kuunga mkono ushahidi wa mtoto sio jambo la msingi na mahakama inaweza kumtia hatiani mshtakiwa ikiwa mahakama itajiridhisha kikamilifu kwamba mtoto husika alikuwa akisema ukweli tena ukweli mtupu.

Ni ipi nafasi ya shahidi mwenye ulemavu wa kuongea na kusikia?

Mtu mwenye ulemavu wa kuongea au kusikia anao uwezo wa kutoa ushahidi mahakamani kwa njia ambayo itamfanya aeleweke kama kwa kutumia maandishi, alama au ishara zitakazo wasilishwa katika mahakama ya wazi.

Mashahidi walio katika mazingira hatarishi au mazingira ya vitisho wanalindwaje?

Mashahidi walio katika mazingira hatarishi au mazingira ya vitisho wanalindwa na Sheria ya Ushahidi kwa namna zifuatazo:

a. Kutokuwakutanisha ana kwa ana shahidi na mshitakiwa wakati wa kutoa ushahidi.
b. Kutoa ushahidi moja kwa moja kwa njia ya mtandao.
c. Kutoa ushahidi kwa njia ya siri.
d. Kutoa ushahidi uliorekodiwa kwa njia ya video katika mahojiano makuu.
e. Kutoa ushahidi kwa njia ya mahojiano kwa kupitia mtu wa tatu.

Shahidi wangapi wanatosha kutoa ushahidi katika kuthibitsha tukio mahakamani?

Sheria ya Ushahidi haishurutishi idadi maalumu ya mashahidi katika kuthibitisha tukio lolote linalobishaniwa; shahidi mmoja anatosha kuthibitisha jambo mbele ya mahakama.

Ushahidi unatolewaje mahakamani katika kuthibisha tukio?

Matukio yote huthibitshwa mahakamani kwa kupitia njia ya mdomo isipokuwa matukio yalioandikwa au matukio yaliyo kwenye kumbukumbu za kielektroniki.

Ushahidi wa mdomo unatakiwa uweje?

Ushahidi wa mdomo unatakiwa uwe wa moja kwa moja kutoka kwa mtu alieona, au alielisikia tukio, alielihisi tukio kwa moja ya viungo vyake vya hisia kama vile ngozi na pua, au awe ni mtu alietoa maoni katika tukio fulani.

Je mtu alie nje ya mahakama au nje kabisa ya Zanzibar anaweza kutoa ushahidi wake?

Ndio, mtu alie nje ya mahakama au nje kabisa ya Zanzibar anaweza kutoa ushahidi wake kupitia video mubashara.

Matukio yalioandikwa yanathibitishwaje mahakamani?

Matukio yalioandikwa huthibishwa mahakamani kwa kupitia hati halisi na zisipokuwepo huthibishwa kwa kutumia vivuli vya hati halisi.

Ushahidi wa kielekroniki ni upi?

Ushahidi wa kielektroniki ni taarifa iliyomo katika kumbukumbu za kielektroniki ambayo imenakiliwa katika karatasi, kuhifadhiwa au kunakiliwa katika kioo au chombo cha kunasa habari kilichotolewa kwa kompyuta ambayo inajulikana kama vifaa vya komputa itachukuliwa kuwa pia ni waraka.

Maoni ya shahidi mtaalamu

Shahidi mtaalamu ni shahidi yeyote mwenye ujuzi au taaluma katika eneo la sheria za kigeni, sayansi, sanaa, au utambuzi wa maandishi, au juu ya alama za vidole. Shahidi mtaalamu hutokea mahakamani pale ambapo mahakama inahitaji maoni yake ya kitaalamu.

Kwa nini maoni ya shahidi mtaalamu ni muhimu?

Maoni ya shahidi mtaalamu yanahitajika mahakamani ili kuweza kuisaidia mahakama katika kufikia maamuzi yake pale ambapo ujuzi na taaluma ya eneo fulani ni muhimu. Mfano wa

wataalamu ni pamoja na madaktari wanaowachanguza waathirika wa kesi za udhalilishaji na wakajaza PF3.

Shahidi anatoaje ushahidi wake mahakamani?

Makamani, shahidi hutoa ushahidi wake kwa mtindo wa mahojiano ambayo yanaweza kufanywa kwa namna tatu ambazo ni:

a. Mahojiano makuu ambapo shahidi huhojiwa na mtu aliyemuita kumtolea ushahidi;
b. Mahojiano kinzani ambapo shahidi huhojiwa na mshatkiwa au mdaiwa baaada ya ; na mahojiano makuu.
c. Mahojiano rejea ambapo shahidi huhojiwa tena na mtu aliyemuita kumtolea ushahidi baada ya mahojiano kinzani.

Je, mke na mume wanaweza kutoleana ushahidi mahakamani?

Ndio, mke na mume wanaweza kutoleana ushahidi ikiwa kuna kesi baina yao au ikiwa kuna kesi ambapo mmoja wao ameshitakiwa kwa kosa la jinai. Hata hivyo, mke na mume hawawezi kulazimishwa kutoleana ushahidi kwa jambo lolote walilowasiliana wakati wa ndoa au hata baada ya ndoa kuvunjika isipokuwa mwanandoa husika au wakala wake kimaslahi awe ameridhia.